

HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

Simu Mkurugenzi : 255(28) 2501375
Ofisi zote : 255 (28) 40334
Fax : 255 (28) 2500785
E-mail. cd@mwanzacc.go.tz
info@mwanzacc.go.tz



S. L.P. 1333
MWANZA.
TANZANIA

Kumb Na. E.30/1/Vol. IX/ 20

3 Novemba, 2017

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA (DIRECTION CLERK)

1. Msimamizi wa Uchaguzi wa JIMBO LA NYAMAGANA
anatangaza

nafasi za kazi ya **KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA
(DIRECTION CLERK)** ambaye atakuwa na jukumu la
kuwaongoza Wapiga Kura wanaokuja kituoni ili wafahamu
mahali/chumba ambacho watapigia kura zao siku ya upigaji
kura tarehe 26 Novemba, 2017.

2. MAJUKUMU MAKUU YA KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA

- Atawajibika kwa Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura,
- Kuwapokea Wapiga Kura wanaokuja kituoni na
kuwaelekeza mahali wanapopaswa kupigia kura zao,
- Kuhakiki kadi za Wapiga Kura wasiojua mahali
watakapopigia kura na kulinganisha taarifa hizo na zile
zilizomo katika Orodha ya Wapiga Kura,
- Kutoa kipaumbele kwa Wapiga Kura ambao ni walemavu,
akina mama wajawazito, wagonjwa, wazee na vikongwe,

3. SIFA ZA KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA

- Awe raia wa Tanzania,
- *Ikiwezekana* awe mkazi wa Kata ya MHANDU ambayo

atafanyia kazi ya kusimamia Upigaji Kura na Kuhesabu Kura

- Asiwe Kiongozi au Shabiki wa Chama cha Siasa,
- Awe *Mwadilifu, Mvumilivu, Mpole, Mtiifu, Msikivu* anayeweza kufanya kazi kwa kujituma,
- Awe na elimu ya Kidato cha nne au zaidi na anayeweza kusoma na kuandika vizuri. Pia anayeweza *kuyaelewa Maelekezo* ya Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura,
- Awe na uwezo wa kuelewa vizuri Maelekezo ya Tume yanayohusu Orodha ya Wapiga kura,

4. UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI YA KAZI

Mwombaji anapaswa kuomba nafasi husika akitoa taarifa kamili zinazomhusu kulingana na sifa zilizotajwa na pia akitaja; kazi yake anayofanya hivi sasa, namba yake ya simu, Jimbo na Kata anayokaa.

Aidha, Mwombaji ambatanishe picha moja ya rangi yenye ukubwa wa pasi ya kusafiria (passport size), vyeti na kitambulisho chochote alichonacho.

Waombaji walioajiriwa wapitishie maombi yao kwa Waajiri wao.

Maombi yote yatumwe kwa:-

**Msimamizi wa Uchaguzi,
Jimbo la Nyamagana,
S.L.P. 1333
MWANZA**

Maombi ya nafasi ya kazi husika yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja katika Ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi, Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

**4. MUDA WA MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI
(DEADLINE)**

Muda wa mwisho wa kuwasilisha maombi ya nafasi ya kazi hii ni tarehe 11/11/2017 saa 9:30 Alasiri.

KIOMONI KIBURWA KIBAMBA
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA NYAMAGANA